United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization




# Viongozi wa Kisiasa:

## FAHAMU ZAIDI kuhusu CSE na Huduma Rafiki kwa Vijana!

**_Mustakabali bora, wenye afya kwa vijana!_**

Elimu ya kina ya ujinsia, afya ya uzazi, maadili ya afya na stadi za maisha (CSE) ni taarifa ya kiutamaduni na inayofaa kwa umri ambayo inawafundisha vijana kuhusu masuala ya ujinsia, uhusiano na afya ya uzazi. Ni muhimu na ni vyema ukaiunga mkono.

Ushahidi unaonyesha kwamba CSE inaongeza elimu ya watoto kuhusu VVU, inawasaidia kuchelewa kufanya ngono, kupunguza idadi ya wenzi wa kingono walionao na kuongeza elimu yao na matumizi ya kingamimba wanapotaka kuzuia maambukizo kwa ngono (STIs) na VVU, pamoja na mimba za utotoni.

**_Unga mkono CSE - Saidia viongozi wetu wa baadaye!_**

## *Kwa nini CSE na Huduma rafiki kwa Vijana Vinakwenda Pamoja*

Elimu ya kina ya Ujinsia, afya ya uzazi, maadili ya afya na stadi za maisha (CSE) inahitaji kuungwa mkono kwa taarifa na huduma za afya zinazopatikana, zinazowezekana kumudu na zinazofaa. Vijana na jamii zao wanakuwa katika hatari bila ya bidhaa ambazo zinawasaidia, ikiwemo: kondomu, kingamimba za kisasa, matibabu ya VVU na maambukizo kwa ngono, ushauri wa mimba na matunzo na huduma nyingine. Hii ndiyo maana kujumuisha CSE katika shule na huduma rafiki kwa vijana katika jamii ni njia ya kuimarisha afya kwa muda mrefu katika nchi za mashariki na kusini mwa Afrika

## *Huduma Rafiki kwa Vijana ni Nini (YFS)?*

Huduma rafiki kwa vijana (YFS) zinazingatia uelewa wa kina wa nini ambacho vijana katika jamii yoyote ile au jumuiya wanakitaka na kukihitaji. Zinahusisha afya ya uzazi ya vijana, haki na utofauti.

YFS inajumuisha:

- Unasihi wa ujinsia na afya ya uzazi.
- Unasihi wa uhusiano na ujinsia.
- Unasihi wa unyanyasaji wa kingono.
- Unasihi kuhusu kingamimba na utoaji wa kingamimba, zikiwemo kingamimba za dharura.
- Kuzuia uambukizo kwa ngono (vikiwemo VVU), huduma za upimaji na unasihi.
- Huduma za kutoa mimba (pale ambapo inaruhusiwa kisheria).
- Huduma za kabla na baada ya kujifungua.

Ujinsia na afya ya uzazi (SRH) vinasaidiwa na elimu, ujuzi na uwezo wa kufanya uchaguzi wa kuwajibika, mzuri, na wenye taarifa kamili na salama za ujinsia - ikiwa ni pamoja na kutofanya ngono.

*"Hakuna uaminifu ulio mzuri zaidi kama ule wa dunia ambayo inawafikiria watoto. Hakuna kazi iliyo muhimu zaidi kuliko kuhakikisha kwamba haki zao zinaheshimiwa, kwamba ustawi wao unalindwa, kwamba maisha yao hayana hofu na mahitaji na kwamba wanakua kwa amani."*

***– Kofi A. Annan, Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifal***

## ***Kwa nini Viongozi wa Kisiasa wanapaswa kujihusisha Kusaidia CSE?***

Katika kanda nzima, vijana 52 wanaambukizwa VVU; kati ya maambukizi hayo mapya, 60% ni wanawake vijana. Kuna vijana balehe na vijana milioni 158 mashariki na kusini mwa Afrika, na 40% kati yao hawana elimu ya msingi na njia za kujikinga na VVU, mambukizo kwa ngono (STIs) na hatari za mimba za utotoni.

Serikali yako imeridhia haki za vijana na watoto kupata taarifa shuleni ambazo zinalinda afya zao, na YFS katika jamii; na bado utafiti uliofanywa na UNICEF, UNFPA na UNESCO umeonyesha kwamba kuna upungufu mkubwa kwa kile kinachofundishwa kwa sasa. Huo unajumuisha: taarifa kuhusu afya ya uzazi, ujinsia na uhusiano, taarifa kuhusu kondomu na kingamimba; utoaji wa ujumbe unaochanganya kuhusu jinsia na haki za binadamu; na marejeo ya ujinsia ambayo sio mazuri na yanaleta hofu.

*“Elimu ni silaha yenye nguvu sana ambayo unaweza kuitumia kuibadilisha dunia.”*

***- Nelson Mandela***

## ***Nini wajibu wangu kama kiongozi wa kisiasa?***

*“Jeshi la kondoo linaloongozwa na simba linaweza kulishinda jeshi la simba linaloongozwa na kondoo.”*

***– Methali ya Kighana***

***Saidia utekelezaji wa sera na miongozo:*** Soma na elewa nyaraka za sera ya taifa zinasema nini. Tengeneza mipango ya utekelezaji ya nchi na kuitekeleza. Shawishi kupata msaada na rasilimali unazohitaji.

***Saidia vijana katika upataji wa taarifa, matibabu na matunzo:*** CSE katika shule na YFS katika jamii sio tu kwa ajili ya vijana amilifu kingono. Ni unyanyapaa huu ambao unawaweka hatarini vijana wanaohitaji taarifa. Taarifa sahihi zinazotoka moja kwa moja kwa watoa huduma ya afya zinaweza kuwa na matokeo mazuri sana katika kuhimiza tabia ya afya ya vijana.

***Viongozi wanawalinda wote:*** Ni wajibu wako kuhakikisha kwamba haki zote za watoto na vijana zinaungwa mkono ili waweze kufanya maamuzi kwa kuwa na taarifa na kwa kuwajibika. Kama kiongozi wa kisiasa, unaweza kuongoza njia na kuwashawishi wengine kuunga

mkono CSE kwa watoto na vijana. Hakikisha kwamba miongozo ya taifa na mapendekezo kuhusu CSE katika shule na jamii yanatekelezwa. Mkataba wa Vijana wa Afrika (AYC) wa mwaka 2006 unaongozwa na dira ya Umoja wa Afrika ya kuhimiza na kusisitiza umuhimu wa vijana kwa maendeleo ya Afrika.

## *Ninaweza Kufanya Nini Kusaidia Kama Kiongozi wa Kisiasa?*

- ***Saidia utekelezaji wa sera na miongozo:*** Soma na elewa nyaraka za sera ya taifa zinasema nini. Tengeneza mipango ya utekelezaji ya nchi na kuitekeleza. Shawishi kupata msaada na rasilimali unazohitaji.
- ***Saidia vijana katika upataji wa taarifa, matibabu na matunzo:*** CSE katika shule na YFS katika jamii sio tu kwa ajili ya vijana amilifu kingono. Ni unyanyapaa huu ambao unawaweka hatarini vijana wanaohitaji taarifa. Taarifa sahihi zinazotoka moja kwa moja kwa watoa huduma ya afya zinaweza kuwa na matokeo mazuri sana katika kuhimiza tabia ya afya ya vijana.
- ***Viongozi wanawalinda wote:*** Ni wajibu wako kuhakikisha kwamba haki zote za watoto na vijana zinaungwa mkono ili waweze kufanya maamuzi kwa kuwa na taarifa na kwa kuwajibika. Kama kiongozi wa kisiasa, unaweza kuongoza njia na kuwashawishi wengine kuunga mkono CSE kwa watoto na vijana. Hakikisha kwamba miongozo ya taifa na mapendekezo kuhusu CSE katika shule na jamii yanatekelezwa. Mkataba wa Vijana wa Afrika (AYC) wa mwaka 2006 unaongozwa na dira ya Umoja wa Afrika ya kuhimiza na kusisitiza umuhimu wa vijana kwa maendeleo ya Afrika.

***Watoto na Vijana Waliopewa taarifa za kutosha:***
***Uchaguzi wenye taarifa za Kutosha - Unaweza Kuongoza Njia!***

United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
SWEDEN
Norad
SAfAIDS
Knowledge for action: The power to make a difference!

**Ofisi ya Kanda ya SAfAIDS, Zimbabwe**:

Barabara ya 17 Beveridge, Avondale, S.L.P A509, Avondale, Harare, Zimbabwe

Simu: +263 4 336 193/4, Faksi: +263 4 336 195

**Tovuti: www.safaids.net**